# LUGHA YA KISWAHILI

# KIDATO CHA TATU S.3 NOTES

## 1. NYAKATI /NJEO – (TENSES);

### Hali ya kukubali (Affirmative form) na
### Hali ya kukanusha (Negative form).;

**KUKANUSHA (NEGATIVES)**

Katika Kiswahili 'Ha' na 'Si' hutumiwa kukanusha. In Kiswahili "HA" and "SI" are used to show the negative.

| KISWAHILI | ENGLISH |
|---|---|
| Mvulana analala | Boy is sleeping |
| Mvulana halali | A boy is not sleeping |
| Msichana anacheza | The girl is playing |
| Msichana hachezi | The girl is not playing |
| mtoto analia | The child is crying |
| mtoto halii | The child is not crying |
| Ninasoma | I am reading |
| Sisomi | I am not reading |
| Mary anatoroka | Mary is escaping |
| Mary hatoroki | Mary is not escaping |
| Rehema anfundishi | Rehema is teaching |
| Rehema hafundishi | Rehema is not teaching |
| Ninaenda nyumbani | I am going home |
| Siendi nyumbani | I am not going home |
| Ninasoma hadithi | Am reading a story |
| Sisomi hadithi | Am not reading a story |
| Ninapenda kula | I love eating |

| | |
|---|---|
| Sipendi kula | I do not love eating |
| Ninataka maji | I want water |
| Sitaki maji | I don’t want water |
| Ninalala | Am sleeping |
| Silali | Am not sleeping |

| **Wakati uliopo. –na-** | **Wakati uliopita. –Li-** | **Wakati ujao. –ta-** | **Wakati uliopo hali timilifu. –me-** |
|---|---|---|---|
| **1. Ninasoma barua.**<br>➢ I am reading a letter<br>**-Sisomi barua.**<br>➢ I am not reading a letter | **Nilisoma barua.**<br>➢ I read a letter<br>**-Sikusoma barua.**<br>➢ I did not read a letter | **Nitasoma barua.**<br>➢ I will read a letter<br>**-Sitasoma barua.**<br>➢ I will not read a letter | **Nimesoma barua.**<br>➢ I have read a letter<br>**-Sijasoma barua.**<br>➢ I have not read a letter |
| **2. Tunasoma barua.**<br>-Hatusomi barua. | **Tulisoma barua.**<br>Hatukusoma barua | **Tutasoma barua.**<br>Hatutasoma barua. | **Tumesoma barua.**<br>Hatujasoma barua. |
| **3. Unasoma barua.**<br>-Husomi barua. | **Ulisoma barua.**<br>-Hukusoma barua. | **Utasoma barua.**<br>Hutasoma barua. | **Umesoma barua.**<br>Hujasoma barua. |
| **4. Mnasoma barua.**<br>-Hamsomi barua. | **Mlisoma barua.**<br>Hamkusoma barua. | **Mtasoma barua..**<br>Hamtasoma barua. | **Mmesoma barua.**<br>Hamjasoma barua. |
| **5. Anasoma barua.**<br>-Hasomi barua. | **Alisoma barua.**<br>-Hakusoma barua. | **Atasoma barua. .**<br>Hatasoma barua. | **Amesoma barua.**<br>Hajasoma barua. |
| **6. Wanasoma barua.**<br>-Hawasomi barua. | **Walisoma barua.**<br>Hawakusoma barua | **Watasoma barua.**<br>Hawatasoma barua. | **Wamesoma barua.**<br>Hawajasoma barua. |

## D) NYAKATI /NJEO;

## Hali ya kukubali na hali ya kukanusha katika nyakati /njeo saba

| **Wakati uliopo.** | **Wakati uliopita.** | **Wakati ujao.** | **Wakati uliopo hali timilifu** | **Wakati uliopita hali timilifu** | **Wakati uliopita hali ya kuendelea** | **Wakati wa mazoea.** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1.Ninaomba**<br>-Siombi | **Niliomba.**<br>-Sikuomba. | **Nitaomba.**<br>-Sitaomba | **Nimeomba.**<br>-Sijaomba | **Nilikuwa nimeomba.**<br>-Sikuwa nimeomba./ | **Nilikuwa ninaomba.**<br>-Sikuwa ninaomba/ | **Mimi huomba**<br>-Mimi huwa siombi. |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **-**Nilikuwa sijaomba | **-**Nilikuwa siombi | |
| **2.Tunaomba**<br><br>**-**Hatuombi | **Tuliomba**<br><br>Hatukuomba | **Tutaomba**<br><br>Hatutaomba | **Tumeomba**<br><br>Hatujaomba | **Tulikuwa tumeomba**<br><br>Hatukuwa tumeomba/<br><br>Tulikuwa hatujaomba | **Tulikuwa tunaomba**<br><br>Hatukuwa tunaomba/<br><br>Tulikuwa hatuombi | **Sisi huomba.**<br><br>Sisi huwa hatuombi |
| **3.Unalima**<br><br>-Hulimi. | **Ulilima**<br><br>-Hukulima. | **Utalima.**<br><br>Hutalima**.** | **Umelima.**<br><br>Hujalima. | **Ulikuwa umelima.**<br><br>-Hukuwa umelima/<br><br>-ulikuwa hujalima | **Ulikuwa unalima.**<br><br>Hukuwa unalima./<br><br>Ulikuwa hulimi. | **Wewe hulima.**<br><br>Wewe huwa hulimi |
| **4.Mnalima**<br><br>-Hamlimi | **Mlilima**<br><br>-Hamkulima | **Mtalima.**<br><br>Hamtalima**.** | **Mmelima.**<br><br>Hamjalima. | **Mlikuwa mmelima.**<br><br>-Hamkuwa mmelima./<br><br>-Mlikuwa hamjalima | **Mlikuwa mnalima.**<br><br>Hamkuwa mnalima./<br><br>Mlikuwa hamlimi. | **Ninyi hulima.**<br><br>Ninyi huwa hamlimi |
| **5.Anakataa**<br><br>-Hakatai | **Alikataa**<br><br>-Hakukataa. | **Atakataa.**<br><br>Hatakataa | **Amekataa.**<br><br>Hajakataa. | **Alikuwa amekataa.**<br><br>-Hakuwa amekataa/<br><br>-Alikuwa hajakataa. | **Alikuwa anakataa.**<br><br>Hakuwa anakataa./<br><br>Alikuwa hakatai. | **Yeye hukataa.**<br><br>Yeye huwa hakatai |
| **6.Wanakataa**<br><br>**-**Hawakatai | **Walikataa**<br><br>Hawakukataa | **Watakataa**<br><br>Hawatakataa | **Wamekataa.**<br><br>Hawajakataa | **Walikuwa wamekataa**<br><br>Hawakuwa wamekataa<br><br>Walikuwa hawajakataa | **Walikuwa wanakataa**<br><br>Hawakuwa wanakataa<br><br>Walikuwa hawakatai | **Wao hukataa.**<br><br>Wao huwa hawakatai |

## VIULIZI (INTERROGATIVES)

Ni maneno ambayo hutumiwa wakati wa kuuliza maswali mf

1. **Kwa nini (why)**

   i Kwanini unacheka?

   Why are you laughing?

   ii Kwa nini unalia?

Why are you crying?

**2. Nani (Who)**

i Nani analala?

Who is sleeping?

ii Nani anaongea?

Who is talking?

**3. Nini (what)**

i Unataka nini?

What do you want?

ii Unapenda nini?

What do you like or love?

**4. Lini (when)**

i Lini utaenda nyumbani?

When will you go home?

ii Lini utanunna gari?

When will you buy a car?

**1. Wapi (where)**

i Unaenda wapi?

Where are you going?

ii Unaishi wapi?

Where do you stay?

**2. Ngapi /Wangapil / Vingapi /Mingapi)**

i. Una pesa ngapi?

How much money do you have?

ii. Una meza ngapi?

How many tables do you have?

iii. Una watoto wangapi?

How many children do you have?

iv. Una wanafunzi wangapi?

How many students do you have?

v. Una visu vingapi?

How many knives do you have?

vi. Una vitabu vingapi?

How many books do you have?

vii. Una milango mingapi?

How many doors do you have?

**VIONYESHI (DEMONSTRATIVES) THIS, / THAT/ THESE/THOSE**

Haya ni maneno ambayo hutumiwa kuonyesha ukaribu ama umbali wa nomino husika km**(Huyu, hawa, huyo, hao, Yule, wale) (Ngeli Ya A - Wa)**

**Huyu**

i Huyu mvulana ni mrefu

This boy is tall

ii Wale wavulana ni werefu

These boys are tall

iii Huyo msichana ni mrembo

That girl is beautiful

iv Hao wasichana ni warembo

Those girls are beautiful

**Yule**

i Yule mvulana ni mpole

That boy is humble

ii Wale wavulana ni wapole

Those boys are humble

**(Hiki, Hivi, Kile, Vile, Hicho, Hivyo)(Ngeli Ya Ki - Vi)**

i. Hiki ni kitabu

This is a book

ii. Vitabu hivi ni vikubwa

These books are big

iii. Kiti hicho ni changu.

That chair is mine

iv. Visu vile ni vyetu

Those chairs are ours

v. Kisu kile ni kikali

That knife is sharp

vi. Visu vile ni vikali

Those knives are sharp

**(Huu hii huo, hiyo ule,ile) (Ngeli ya U - I)**

i Mikate hii ni mitamu

These loaves of bread are sweat

ii Mti ule ni mrefu

That tree is tall

iii Miti ile ni mirefu

Those trees are tall

**(Hii-hizi hiyo, zile, ile, zile)(Ngeli ya U - Zi)**

i. Hii meza ni yangu

This table is ours

ii. Kalamu ile ni mpya

That pen is new

iii. Kalamu zile ni mpya

Those pens are new

**(Hili, yale, ile yale)(Ngeli ya Li - Ya)**

**Hili**

i. Jiwe hili ni langu

This stone is mine

ii. Mawe yale ni yetu

Those stones are ours

iii. Jembe lile ni kubwa

That hoe is big

iv. Majembe yale ni makubwa

Those hoes are big

**VIWAKILISHI (PERSONAL PRONOUNS)**

Ni maneno ambayo hutumwa kuwakilisha nomino

1. Mimi(I am)

i. Mimi ni msichana mfupi

I am a short girl

ii. Mimi ni mvulana mfupi

I am a short boy

**2. Wewe (you)**

i Wewe ni mwanafunzi

You are a student

ii Wewe ni mama yangu

You are my mother

**3. Yeye (she /he)**

i Yeyeni mkulima

She/he is a farmer

ii Yeye ni mwanafuzi mzuri

She /he is a good student

**4. Sisi (we)**

i Sisi ni watoto wa Mungu

We are children of God

ii Sisi ni wanafunzi werevu

We are bright students

**5. Wao(they)**

i Wao ni wakristo

They are Christians

ii Wao ni walimu wetu

They are our teachers

**6. Nyinyi (you plural)**

i Nyinyi ni watumishi wa mungu

You are servants of God

ii Nyinyi ni watoto wangu

You are my children

**NYAKATI TENSES (Na) (PRESENT TENSE)**

i Ni<u>na</u>enda mjini

Iam going to town

ii Ni<u>na</u>nunua kitabu

I am buying a book

iii Ni<u>na</u>enda nyumbani

Iam going home

iv Ni<u>na</u>kula chakula

Iam eating food

**WAKATI UJAO(Ta)/FUTURE TENSE**

i Ni<u>ta</u>lala jioni

I will sleep in the evening

ii Ni<u>ta</u>kimbia nikiona nyoka

I will ran if I see a snake

iii Ni<u>ta</u>kunywa chai asubuhi.

I will take tea in the morning

**WAKATI ULIOPITA(Li)(PAST TENSE)**

i Ni<u>li</u>enda Kampala

I went to Kampala

ii Nilinunua kalamu

I bought a pen

iii Nilienda shule

I went to school

**WAKATI TIMILIFU (Me) (PRESENT PERFECT TENSE)**

i Nimefunza hesabu

I have taught mathematics

ii Nimepata kazi

I have got a job

iii Nimesoma hadithi nzuri

I have read a nice story

**KUMILIKI WAKATI ULIOPO/TO HAVE PRESENT TENSE**

(a**) Nina (I have)**

i Nina watoto wawili

I have two children

ii Nina viti viwili

I have two chairs

iii Nina vitanda vinne

I have four beds

(b) **Una (you have)**

- Una miti mitano

  You have five trees

- Una nyumba mbili

  You have two houses

- Una kalamu nne

  You have four pens

**c) Ana (he /she has)**

- Ana chakula kingi

She/he has a lot of food

- Ana nguo nzuri

  She /he has a nice clothe

- Ana gari kubwa

  He/she has a big car.

**d) Tuna (we have)**

- Tuna wazazi wazuri

  We have nice /good parents

- Tuna walimu wengi

  We have many teachers

- Tuna Shule Kubwa

  We have a big school

**e) Wana (they have)**

- wana vitabu vizuri vya hadithi

  They have good story books

- wana nyumba kubwa

  They have a big house

**KUMILIKI WAKATI ULIOPITA/TO HAVE PAST TENSE KUMILIKI**

**a) Nilikuwa na: (I had)**

i. Nilikuwa kitabu

   I had a book

ii. Nilikuwa na pesa nyingi

   I had a lot of money

iii. Nlikuwa na chakula

   I had food

iv. Nilikuwa na gari

   I had a car

**(b)Ulikuwa na (you had)**

i Ulikuwa na maziwa

You had milk

ii Ulikuwa na pombe

You had Alcohol

iii Ulikuwa na kalamu

You had a pen

iv Ulikuwa na magari

You had cars

C**. Alikuwa na (she /he had)**

i Alikuwa na asali

He/she had honey

ii Alikuwa na baisikeli

He/she had a bicycle

iii Alikuwa na kijiko

He/she had a spoon

iv Alikuwa na nguo nzuri

He/she had nice clothe

**d). Tulikuwa na (we had)**

i Tulikuwa na wanafunzi wazuri

We had good students

ii Tulkuwa na chakula cha kutosha

We had enough food

iii Tulikuwa na wazazi wema

We had good parents

iv Tulikuwa na ugali

We had posho

**e) Walikuwa na (they had)**

i Walikuwa na farasi

They had a horse

ii Walikuwa na shamba kubwa

They had a big farm

iii Walikuwa na viti vingi

They had many chairs

iv Walikuwa na wageni jana

They had visitors yesterday

**UMOJA NA WINGI/SINGULAR PLURAL**

**Ngeli ya (M -Wa,{A - WA})**

Ngeli hii hutumiwa kuonyesha, wanyama (watu).”m” hutumwa kuonyesha umoja na “wa’ katika wingi

| **Kiswahili** | **Wing** | **Singular** |
|---|---|---|
| Mtu | Watu | A parent |
| Mwanaume | Wanaume | Man |
| Mwanamke | Wanawake | Woman |
| Mgeni | Wageni | Vsitor |
| Mtoto | Watoto | A child |
| Mvulana | Wavulana | A boy |
| Msichana | Wasichana | A girl |
| Mwalimu | Walimu | A teacher |
| Mwanafunzi | Wanafunzi | A student |
| Mwizi | Wezi | A thief |

**Matumizi/Use**

<u>Umoja</u>

Mtoto analala

The child is sleeping

<u>Wingi</u>

Wavulana wanacheza

The boys are playing

Umoja

Mwanafuzi anasoma kitabu

The student is reading a book

Wing

Wanafunzi wanasoma vitabu

The students are reading books etc

**(ii) Ngeli ya –m-mi(U-I)**

Nomino katika kikundi hiki katika umoja huanza na "m na katika umoja, na huanza na Mi' katika wingi

| **Kiswahili** | | **English** |
|---|---|---|
| Umoja | Wingi | Singular |
| Mti | Miti | A tree |
| Mlango | Milango | Door |
| Mkate | Mikate | Bread |
| Mkebe | Mikebe | Tin |
| Mkuki | Mikuki | Spear |
| Msitu | Misitu | Bush |
| Mguu | Miguu | Leg |
| Mkono | Mikono | Hand |
| Mmea | Mimea | Plant |
| Mkeka | Mikeka | Mat |
| Mto | Mito | River |

**Matumizi/Use**

**Umoja**

Mti wangu

My tree

**Wingi**

Miti yetu

Our trees

**Umoja**

Mkono wangu ni mfupi

My hand is short

Mikono yetu ni mifupi

Our hands are short

**Umoja**

Mkate wa Joshua umeharibka

Joshua's bread has gone bad

**Wingi**

Mikate ya Joshua imeharibika

Joshua's loaves of bread have gone bad

**(iii) Ngeli ya Ki-Vi**

Nomino katika ngeli hi huanza na 'Ki' Katika umoja na 'Vi' katika wingi

| **Kiswahili** | | **English** |
|---|---|---|
| **Umoja** | **Wingi** | **Singular** |
| Kitabu | Vitabu | Book |
| Kisu | Visu | Knife |
| Kichwa | Vichwa | Head |
| Kikombe | Vikombe | Cup |
| Kitanda | Vitanda | Bed |
| Kipepeo | Vipepeo | Butterfly |

| | | |
|---|---|---|
| Kiti | Viti | Chair |
| Kijana | Vijana | Youth |
| Kiongozi | Viongozi | Leader |
| Kijiko | Vijiko | Spoon |
| Kidole | Vidole | Finger |
| Kifua | Vifua | Chest |

**Matumizi/Use**

**Umoja**

Kitabu changu

My book

**Wingi**

Vitabu vyetu

Our books

**Umoja**

Kisu hiki ni kizuri

This knife is nce

**Wingi**

Visu hivi ni vizuri

These knives are nice

**Umoja**

Kikombe changu kilipotea

My cup got lost

**Wingi**

Vikombe vyetu villipotea

Our cups got lost.

**(iv). Ngeli ya U-N(U-Zi)**

Nomino katika ngeli hii hazina umbo maalum katika umoja au wingi/Nouns in this class are irregular nouns and do not have a specific form in singular and plural in Kiswahili.

| **Kiswahili** | | **English** |
|---|---|---|
| Uso | Nyuso | Face |
| Uzi | Nyuzi | Thread |
| Ufa | Nyufa | Crack |
| Ukuta | Kuta | Wall |
| Ukurasa | Kurasa | Page |
| Ufalme | Falme | Kingdom |
| Upande | Pande | Side |
| Ulimi | Ndimi | Tongue |
| Ufunguo | Funguo | Key |

**Matumizi/Use**

i Ufunguo wangu ulipotea (my key got lost

Funguo zetu zilipotea

ii Ulimi wako utakusaliti

Your tongue will betray you?

iii Ndimi zenu zitawasaliti

Your tongues will betray you?

**Ngeli ya (I-I)**

Kikundi hiki kina baadhi ya maneno ambayo hayahesabiki/ This class has some uncountable words

| Kiswahili | | English |
|---|---|---|
| **Umoja** | **Wingi** | |
| Sukari | Sukari | Sugar |
| Chumvi | Chumvi | Salt |
| Mvua | Mvua | Rain |

| | | |
|---|---|---|
| Asali | Asali | Honey |

**Matumzi ngeli ya (I-I)**

i Mtoto alimwaga sukari

The child poured sugar

Watoto walimwaga sukari

Children poured sugar

ii Mvua ilinyesha jana

It rained yesterday

**Ngeli Ya J-Ma (Li-Ya)**

Baadhi ya maneno katka kikundi hiki huanza kwa herufi ‘J’ katika umoja (singular) na ‘Ma’ kwa wingi (plural)

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Jicho | Macho | Eye |
| 2. | Jina | Majina | Name |
| 3. | Jembe | Majembe | Hoe |
| 4. | Jeshi | Majeshi | Army |
| 5. | Jibu | Majibu | Answer |
| 6. | Jiwe | Mawe | Stone |
| 7. | Jivu | Majivu | As |
| 8. | Jumba | Majumba | Bg house |
| 9. | Jino | Meno | Tooth |
| 10. | Sikio | Masikio | Ear |

**Matumizi/Use**

1. Jembe langu ni kubwa (My hoe is big)

   Majembe yetu ni makuwa (Our hoes are big)

2. Jina lako ni nzuri (your name is good)

Majina yetu ni mazuri (Our names are good)

**VIELEZI (ADVERBS)**
**VIELEZI VYA JINSI /NAMNA /ADVERS OF MANNER)**

1. **Pole Pole (Slowly)**

i Mtoto anatembea polepole (The child is walking slowly)

ii Mzee anacheza polepole (The old man is playing/dancing slowly)

iii Dada yangu anacheka polepole (My sister is laughing slowly)

2. **Upesi (quickly)**

i Huyu mvulana anatembea upesi (This boy is walking quickly)

ii John anaandika upesi

iii Baba anakula upesi

iv Patricia anacheza upesi

v Moses anakimbia upesi

3. **Vibaya (badly)**

i Wanafunzi walifanya kazi vibaya (Students did the work badly)

ii Okello anacheza vibaya

iii Paparu alianguka vibaya

iv Mtotoaliumia vibaya

4. **Ghafla (suddenly)**

   i Dereva alilisimamisha gari ghafla (The driver stoped the car suddenly)

   ii Ajali ilitokea ghafla

   iii Adamba alianguka ghafla

   iv Mto ulikauka ghafla

   v Nyumba ilishika moto ghafla

5. **Vizuri (properly / well )**

   i Mwalimu aliniambia nivae vizuri (The teacher told me to dress properly)

   ii Patricia anaandika vizuri

   iii Enock alitembea vizuri

6. **Salama (safely) (well)**
    i. Wageni walifika salama (The visitors reached safely)
    ii. Wanafunzi walifika mjini salama
    iii. Nililala salama

**VIELEZI VYA MAHALI (ADVARBS OF PLACE)**

1. **Karibu (near)**

i. Mtoto alisimama karibu na nyoka (The child stood near the snake)
ii. Mwanafunzi alikaa karibu na mwalimu
iii. Mama yangu alienda karibu na mto

2. **Nje (Out Side)**

i. Mama yangu alienda nje ya nyumba usiku (My mother went outside the house in the night)
ii. John alienda nje ya nchi
iii. Nimesimama nje ya darasa

3. **Nyuma ya (behind)**

i. Mwanafunzi alienda nyuma ya shule (The student went behind the school)
ii. Mtoto aliketi nyuma ya meza
iii. Mbwa alikufia nyuma ya choo
iv. Baba amesimama nyuma ya zizi

4. **Chini ya (Under)**

i. Mtoto alilala chini ya kitanda (The child slept under the bed)
ii. Baba yangu analala chini ya mti
iii. Paka amelala chini ya meza

5. **Juu ya (On top of)**

i. Alice alipanda juu ya meza (Alice climbed on top of the table)
ii. Mtoto alilala juu ya kitanda
iii. Kuku amepanda juu ya mti

6. **Mbali (far…….)**

i Kutoka hapa hadi Nairobi ni mbali (From her to Nairobi is far)

ii Baba yangu alienda mbali

iii Shule yangu inapatika na mbali

iv Kaka anaishi mbali na sisi

**VIELEZI YYA WAKATI (ADVARBS OF TIME)**

**1. Asubuhi (Morning)**

i Mwanafunzi alienda shuleni asubuhi

**ii** Mtoto aliamka asubuhi

iii Nilienda shambani asubuhi

**2. Leo (Today)**

i Leo nitakula chakula kingi

ii Leo nitasoma Kiswahili

iii Leo nitaenda kanisani

**3. Mapema (very early)**

i Nitakula chakula mapema

ii Nitalala mapema

iii Nitaenda darasani mapema

**4. Hivi punde(Right now/very soon)**

i Rais wetu atawasili hivi punde

ii Nitarudi nyumbani hivi punde

iii Nitapka chakula hivi punde

**5. Jioni (Evening)**

i Baba atarudi jioni kutoka kazini

ii Tutatazama kipindi jioni

iii Mimi nitakula chakula jioni

**6. Usiku (night)**

i Kaka alisafiri usiku

ii Victoria alitembea usiku

iii Dada atapika chakula usiku

**VIUNGANISHI (CONJUCTIONS)**

Viunganishi ni maneno ambayo huunganisha sentensi

1. **Na (and)**
   - i Juma na John wanaenda shuleni
   - ii Msichana na mvulana wanacheza
   - iii Mwalimu na watoto wanakula wali
2. **Lakni (but)**
   - i John analia lakini James anacheka
   - ii Mary anasoma lakini Jane analala
   - iii Pauline ni rafiki yangu lakini Sudat ni adui yangu
   - iv Kaka yangu alichapwa na baba kwa sababu ni mjeuri
   - v Mwalimu anafundisha kwa sababu anataka wanafunzi wake wapite mtihani
3. **Kuwa/Kwamba(that )**
   - i Baba yangu alisema kuwa ataenda shuleni
   - ii Mwalimu alisema kuwa sisi ni wanafunzi wazuri
   - iii Mama yangu alisema kwamba ataninunulia nguo nzuri kesho
   - iv Dada alituahidi kuwa ataimba wimbo.
4. **Pia (Also)**
   - i Mama yangu anafua nguo pia mama yako.
   - ii Pia mimi nitaenda mjini na kaka yangu
   - iii Baba pia mama watasafiri mjini
5. **Ama, au(or)**
   - i Unataka maziwa au asali?
   - ii Unataka kalamu au kitabu?
   - iii Unataka kwenda nyumbani au utabaki shuleni?
   - iv Utaenda Nairobi ama Mombasa?

v Unampenda mama au babu?

vi Unapenda kula kuku au nyama?

**MAGONJWA (DISEASES)**

| **KISWAHILI** | **ENGLISH** |
|---|---|
| Homa | Cough |
| Kisonono | Gonorrhea |
| Kichwa kuuma | Headache |
| Kuhara | Diarrhoea |
| Ugonjwa wa kifua / Kifua kikuu | Tuberculosis |
| Surua /ukambi | Measles |
| Ndui | Smallpox |
| Tauni | Plague |
| Kipindupindu | Cholera |
| Kaswende | Syphilis |
| Unyafuzi/Utapia mlo | Kwashiorkor |
| Kiarusi | Polio |
| Kisukari | Diabetes |
| Ukimwi | AIDS |
| Homa ya manjano | Yellow fever |
| Homa ya malaria | Malaria fever |
| Kifaduro | Whooping cough |
| Ukoma | Leprosy |
| Matubwitubwi | Mumps |
| Kohozi | Cough |
| Kichocho | Bilharzia |
| Malale | Sleeping sickness |
| Kifafa | Fits |

| | |
|---|---|
| Pepopunda | Tetanus |
| Vidonda | Wounds |
| Kansa | Cancer |
| Pumu | Asthma |
| Tezi | Goiter |
| Ugonjwa wa matende | Elephantiasis |
| Mafua | Flue |

**VILEMA (PEOPLE WITH DEFECTS)**

| **Kswahili** | **English** |
|---|---|
| Kiziwi | A deaf person |
| Kiwete | A lame person (both legs) |
| Kikono | A person with only one hand lamed |
| Kipofu | A blindperson |
| Bubu | A dump person |
| Chongo | One eyed person |
| Kibiongo / kijongo | A person with a hump on the back |
| Kibogoyo | Toothless person |
| Kengeza/jicho | Failure of the eyes to look at something directly. |
| Kiguru /Kiguu | A lame person (only one leg affected) |
| Zeruzeru | Albino |
| Kigugumizi | Stamerer |

**Matumizi (Use)**

1. Kiziwi Yule anaugonjwa wa kisukari

   That deaf person is suffering from diabetes
2. Yule kipofu ni jirani yangu
3. Chongo alinitembelea leo asubuhi

**VIVUMISHI/SIFA (ADJECTIVES)**

Haya maneno ambayo hutoa habari zaidi kuhusu nomin km

1. **Mwaminifu (Honest /faithful)**
   - i Mary ni mke mwaminifu

     Mary is a honest wife
   - ii Peter ni mwanafuni mwaminifu

     Peter is a faithful boy
   - iii. Huyu msichana ni mwaminifu

**2. Mpole (humble /polite)**

- i Jane ni msichana mpole

  Jane is a humble girl
- ii Dada yangu ni mpole

  My sister is humble
- iii Huyu mtalii ni mwaminifu

**3. Mrembo (beautiful)**

i James ana mke mrembo

James has a beautiful wife

ii Yule msichana ni mrembo

That girl is beautiful

**iii** Juma ana mtoto mrembo

4. **Mrefu (tall**)

i Baba yangu ni mwanamume mrefu

My father is a tall man

ii Shangazi yangu ni mwanamke mrefu

My aunt is a tall woman

iii Mwalimu wetu wa hesabu ni mrefu

**5. Mfupi (short)**

i Kaka yangu ni mvulana mfupi

My brother is a short boy

ii Mjomba wangu ana mtoto mfupi

My uncle has a short child.

iii Binamu yangu ni mfupi

**6. Mweupel (light skinned)**

i Mama yangu ni mweupe

My mother is light skinned

ii Patricia ni msichana mwepe

Patricia is alight skinned girl

iii Msichana mweupe hupendeza

**7. Mweusi (dark skinned)**

i Defao ni mwanamume mweusi

Defao is a dark skinned man

ii Rafiki yangu ni mweusi

My friend is dark skinned

iii Yule mwanamke ni mweusi kama mkaa

**8. Mwerevu (bright, intelligent, clever)**

i Salah ni mchezaji mwerevu

Salah is a bright player

ii Wafula ni mwanafunzi mwerevu

Wafula is a bright student

iii Nina mtoto mwerevu

**9. Tajiri (Arich person, country / continent)**

i Uganda ni nchi tajiri

Uganda is a rich country

ii Bara la Afrika ni tajiri

Africa is a rich continent

iii Mwalimu mkuu wetu ni tajiri

Our headteacher is rich

**10. Maskini (a poor person, country, continent)**

i Mzazi wangu ni mtu masikini

My parent is a poor person

ii Babu yangu ni mtu maskini

My grand father is a poor person

iii Nchi ya Somali ni maskini

**11. Mzuri / kizuri / nzuri (nice /good)**

i Binamu yangu ni mtu mzuri

My cousin is a good person

ii Nina kiti kizuri

I have a nice chair

iii Shule yetu ni nzuri

Our school is nice

**VIHUSISHI (PREPOSITIONS)**

Ni neno ama kikundi cha maneno ambayo hutumiwa kuonyesha mahali, nafasi wakati km

1. **Katika (in / on)**

i Mtoto aliweka kikombe katika meza

The child placed the cup on the table

ii Wageni walilala katika chumba kizuri

The visitors slept in a good room

2. **Chini Ya (Under)**

i Mtoto alilala chini ya kitanda

The child slept under the bed

3. **Juu Ya (On Top of……)**

i. Simama juu ya meza

Stand on top of the table

**4. Nyuma ya (behind)**

i. Mfalme alienda nyuma ya kasri yake

The king went behind his palace

**5. Baada ya (after)**

- Ndambuki atalala baada ya kula chakula

  Ndambuki will sleep after eating food

**6. Kabla ya (before)**

- Mashaka alifika shuleni kabla ya asiimwe

  Mashaka reached school before asiimwe

**VIMILIKISHI (POSSESSIVES)**

Haya ni maneno ambayo huonyesha umilikaji kwa mfano

1. **Wangu (my)**

   Wangu hutumika kwenye nominozenye huuanza kwa herufi ‘m’ kwa umoja.

   This is used on nouns that begin with suffix ‘m’ in singular

   **Kwa mfano/For example:**

i Mtoto wangu ni mgonjwa

My child is sick

ii Mwalimu wangu ni mrefu

My teacher is tall

iii Mke wangu ni mrembo

My wife is beautiful

iv Mwanafunzi wangu huaandika vizuri

My student writes well

2. **Changu (mine)**

   Changuhutumika kuonyesha maneno yanayo anza kwa herufi ‘Ki’ katika umoja

   It is used to show words that begin with suffix ‘Ki’ in singular

**Matumizi (Use)**

i Kikombe changu kimepotea

My cup is lost

ii Kitabu changu ni kidogo

My book is small

iii Kidole changu ni kizuri

My finger is nice

iv Kitanda changu nikikubwa

My bed is big

**3. Yangu**

Yangu hutumika kuonyesha manenoambayo hayaweziKuhesabika katika lugha ya Kiswahili

This is used with uncountable words in Kiswahili

**Matumizi(Use)**

i Meza yangu iliibiwa

My table was stolen

ii Mama yangu ni mpole

My mother is polite

iii Shangazi yangu ni mwaminifu

My aunt is trustworthy

iv Nyumba yangu ni kubwa

My house is big

v Kaka yangu atafunga ndoa

My brother will get married.

**4. Wako (yours)**

**Matumizi(Use)**

i Mtoto wako ameumia

Your child is injured

ii Mti wako utakauka

You tree will dry

iii Mzazi wako anakutafuta

Your parent is looking for you

iv Mkeka wako umepigwa na mvua

Your mat has been rained on

v Mkate wako umeoza

Your bread is rotten

vi Msichana wako anatabia nzuri

Your girl is well behaved

**5. Yetu (ours)**

i Maua yetu yamekauka

Our flowers have dried up.

ii Dada yetu atasafiri leo

Our sister will travel today

iii Baba yetu amenunua samaki mtamu sana

Our father has bought a very sweet fish

iv Babu yetu ni mgonjwa

Our grand father is sick

**KINYUME (OPPOSITE)**

| **Kiswahili** | | | **English** | |
|---|---|---|---|---|
| **Neno** | **Kinyume** | | **Word** | **Opposite** |
| Amani | Vita | | Peace | War |
| Mkwasi | Mkata | | Rich person | Poor person |
| Ukweli | Uongo | | Truth | A lie |
| Nyeusi | Nyeupe | | Black | White |
| Funga | Fungua | | Shut | Open |
| Funika | Funua | | Cover | uncover |
| Funga | Fungua | | Close | Open |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Fupi | Ndefu | | Short | Tall |
| Juu | Chini | | Up | Down |
| Bara | Pwani | | Hinterland | Sea |
| Haba | Tele | | Scarce | Abundant |
| Baridi | Joto | | Coldness | Hotness |
| Uhuru | Utumwa | | Freedom | Slavery |
| Utii | Ukaidi | | Obedience | Disobedience |
| Kaka | Dada | | Brother | Sister |
| Mke | Mume | | Wife | Husband |
| Rafiki | Adui | | Friend | An enemy |
| Mchana | Usiku | | Day | Night |
| Mwangaza | Giza | | Light | Darkness |
| Mama | Baba | | Mother | Father |
| Mzee | Kijana | | Old | Youth |
| Chache | Nyingi | | Little | Much |
| Ndoa | Talaka | | Marriage | Divorce |
| Baraka | Laana | | Luck/blessings | Curse |
| Babu | Nyanya /bibi | | Grandfather | Grandmother |
| Fuma | Fumua | | Weave | Unweave |
| Bana | Banua | | Squeeze | Loosen |
| Tega | Tegua | | Set a trap | Remove the trap |
| Cheka | Lia | | Laugh | Cry |
| Penda | Chukia | | Love | hate |
| Enda | Rudi | | Go | Come back |
| Furaha | Huzuni | | Happiness | Sadness |

**Zoezi;**

**Andika sentensi kumi ukitumia vinyume hivyo hapo juu;**

**KUKANUSHA (NEGATIVES)**

Katika Kiswahili ‘Ha’ na ‘Si’ hutumiwa kukanusha. In Kiswahili “HA” and “SI” are used to show the negative.

| **KISWAHILI** | **ENGLISH** |
|---|---|
| Mvulana analala | Boy is sleeping |
| Mvulana halali | A boy is not sleeping |
| Msichana anacheza | The girl is playing |
| Msichana hachezi | The girl is not playing |
| mtoto analia | The child is crying |
| mtoto halii | The child is not crying |
| Ninasoma | I am reading |
| Sisomi | I am not reading |
| Mary anatoroka | Mary is escaping |
| Mary hatoroki | Mary is not escaping |
| Rehema anfundishi | Rehema is teaching |
| Rehema hafundishi | Rehema is not teaching |

| | |
|---|---|
| Ninaenda nyumbani | I am going home |
| Siendi nyumbani | I am not going home |
| Ninasoma hadithi | Am reading a story |
| Sisomi hadithi | Am not reading a story |
| Ninapenda kula | I love eating |
| Sipendi kula | I do not love eating |
| Ninataka maji | I want water |
| Sitaki maji | I don't want water |
| Ninalala | Am sleeping |
| Silali | Am not sleeping |

# BARUA:

**Tofauti na kulingana kuliopo kati ya Barua ya kirafiki na Barua rasmi:**

| BARUA RASMI;- | BARUA YA KIRAFIKI;- |
|---|---|
| • **Anwani** mbili, yaani; ya Mwandishi na Mwandikiwa | • Anwani moja tu. Anwani ya Mwandishi. |
| • **Tarehe** inawekwa chini ya anwani ya Mwandishi. | • Tarehe inawekwa chini ya Anwani ya Mwandishi. |
| • **Mtajo** uwe chini ya anwani ya mwandikiwa:- Bibi/Bwana: | • Mtajo umtambulishe mwandikiwa:- K.m; Kwako Mama, |
| • **Mada**; Barua rasmi sharti iwe na mada.Zingatia sifa zake | • Haina mada kamwe. |
| • **Utangulizi**: Mwandishi anajielezea kwa Mwandikiwa | • Mwandishi antoa salamu kwa Mwandikiwa |
| • **Kiini**: Toa lengo la barua pamoja na tajiriba/uzoefu wako<br>• **Hitimisho**: Weka sahihi &majina yako kikamilifu.<br>***ZOEZI;*** *Tangazo limetokea katika gazeti la Daily monitor likitangaza nafasi ya kazi ya meneja wa kiwanda cha Taifa Ltd. Mwandikie mkurugenzi wa kiwanda hicho ukiomba nafasi ya kazi hiyo.* | • **Kiini**:Toa hoja au mawazo yako mbalimbali.<br>• **Hitimisho**:Weka sahihi &majina<br>***ZOEZI;*** *Mwandikie barua mzazi wako ukimkumbusha mkutano wa wazazi pamoja na kumwomba atakapokuwa akija akuletee mahitaji yako muhimu hapo shuleni.* |

SHULE YA UPILI YA IMANI

S. L. P 72
MBALE
16 – 7 – 2016

**Kwa Baba Mpendwa,**

Shikamoo baba? Ninadhani uhali njema na mola amekupa afya bora. Huku nyumbani mimi, mama na ndugu zangu tuko wazima. Hali imeanza kuwa ngumu kwasababu mama sasa hana kazi na hata hana pesa ambazo anaweza kutumia ili tuendele kuishi vizuri.

Sababu ambayo imenifanya nikuandikie hii barua ni kuwa, shuleni nilifukuzwa kwa ajili ya pesa za mtihani ambao utaanza tarehe ishirini, mwezi wa nane mwaka wa elfu mbili kumi na sita, ikiwa inawezekana ungenitumia pesa ili nikalipe shuleni kwasababu singependa kukosa kufanya huo mtihani.

Nilimweleza mama lakini aliniambia kuwa yeye hana hela kwa hivyo nikaamua kukuandikia barua hii. Upande mwingine kando na hela, ninaendelea vizuri sana na masomo yangu.

Sisi sote nyumbani tuko wazima isipokuwa mama yetu aliyeuguwa kidogo lakini ndugu zetu wakubwa walimpeleka hospitalini na akatibiwa na sasa hivi anahisi vizuri.

Kitu kingine ambacho ningependa kukueleza ni kuwa sisi sote tumengoja siku utakayo rudi nyumbani kwani tutafurahi sana kama vibogoyo waliopata meno wakati wa mlo kwani sisi sote tunatamani kukuona. Toa salamu zetu kwa marafiki wako na kwa shangazi. Mola akubariki na nitafurahi sana kama utazingatia ombi langu.

**Kutoka Kwa Mtoto Wako**

……………………

**Mbilia Bel**

**MASWALI**

i) Ni nani ameandika waraka huu? (Alama 02)

ii) Taja shughuli ya mwandishi wa barua hii. (Alama 02)

iii) Mamake mwandishi wa barua hii ana shida gani? (Alama 04)

iv) Kwanini mwandishi wa barua hii yuko nyumbani sasa? (Alama 06)

v) Mwandishi wa barua hii anahofu nini? (Alama 06)

**FAMILIA YETU**

Jina langu ni Namubi Victoria Adamba, baba yangu ni Zacheria Adamba na mama ni Margret Nandala Adamba. Katika familia yangu tuko watoto wanne, wavulana watatu na msichana mmoja.

Mimi ni kitinda mimba na tena ni msichana pekee. Ndugu yangu mkubwa anaitwa Bosco Bwayo Adamba, na wa pili ni Antonny Mutai Adamba na watatu ni Moses Wafula Adamba.

Mimi na familia yetu tunaishi katika mji mkuu wa Nairobi katika wilaya ya Wilson Airport South C, sisi ni watoto wenye nidhamu.

Katika familia yetu ndugu zangu hufanya kazi mbali mbali kama uawalimu, uhasibu na ujenzi. Ndugu zangu wote wameoa na wana familia zao.

Mimi ni mtoto aliyesalia nyumbani na wajukuu wa wazazi wangu. Katika familia yangu tunapenda kutazama vipindi vya runinga kama michezo haswa ile ya kandanda, kukimbia, kuogelea, mpira wa kikapu na kadhalika.

Pia tunapenda kutazama taarifa ya saa moja na pia ile ya saa tatu. Wazazi wangu hupenda kutazama taarifa ya saa moja.

Katika familia yangu, sisi ni wa dhehebu la kisabato. Sisi huenda kanisani siku ya jumamosi. Tulizaliwa na tukalelewa kwa dini hiyo.

Katika familia yetu sisi tunapenda kula ndizi iliyopikwa na mboga za kienyeji ingawa baba yangu hupenda kula ugali kwa nyama.

Katika familia yangu, wakati wetu wa kupumuzika sisi huenda kutembea katika sehemu mbalimbali kama kwenda kuwaona wanyama wa pori katika mbuga ya wanyama karibu na bustani ya Uhuru.

Katika familia yetu tunaishi kwa amani pamoja na heshima, hatuna ubaguzi wala ukabila.

Tunapenda mataifa yote ya Afrika Mashariki na Afrika nzima. Sisi tunapenda Afrika kwasababu hata sisi ni waafrika.

Tunapenda kusikiliza nyimbo za kidini kama vile za Judith Babirye, Wilson Bugembe, Neema Mwaipopo, Bahati Bukuku, Rose Muhando na zile za wasani wengine.

Katika familia yetu sisi huishi na watu wa ukoo wa baba pamoja na ule wa mama. Tunawapenda watu wote wa hizi koo mbili.

Katika familia yetu kila krisimasi sisi hufanya sherehe na kuwaalika watu wa ukoo wa mama pamoja na ule wa baba ilituweze kujuliana hali pamoja na kujitambulisha.

Mimi ninaipenda familia yangu kwa dhati kwasababu wazazi wetu wanatulea vizuri.

**<u>MASWALI</u>**

i) Familia hii ina watu wangapi? (Alama 02)

ii) Ni nani kitinda mimba katika familia hii? (Alama 02)

iii) Familia hii huishi katika nchi gani? (Alama 02)

iv) Familia hii ni ya dini gani? (Alama 02)

v) Ni funzo gani tunalopata kutoka kwa familia hii? (Alama 02)

## SHULE YANGU

Shule yangu inaitwa Baraka na inapatikana katika wilaya ya Huruma. Kwenye kijiji cha Sungura. Shule hii ina wanafunzi elfu moja na mia moja.

Shule hii ni ya mseto ina wavulana mia sita na wasichana mia tano. Pia ina walimu thelathini na tano, wa kiume ishirini na wa kike ni kumi na tano.

Shule yangu ni kubwa, ina maji, tarakilishi, shule yetu hulisha wanafunzi vyakula vizuri vyenye afya kama maharagwe, ugali, mayai mananasi, wali na vinginevyo.

Shule yangu hucheza michezo ya aina mbalimbali kama kandanda, voliboli, mpira wa kikapu, kuogelea pamoja na michezo mingineyo. Kila jumapili baada ya chakula cha mchana, wanafunzi huenda kwenye viwanja vya michezo tofauti kucheza.

Katika shule yangu, wanafunzi hufunzwa masomo tofauti kama vile Kiswahili, kiingereza, hesabu, masomo ya sayansi na kadhalika.

Sisi tunaabudu Mungu siku ya jumamosi kwani shule ni ya dhehebu la kisabato. Katika shule yetu kuna wanafunzi wengi wa kigeni, kuna watokao katika nchi ya Kenya, Tanzania, Rwanda na pia Kongo.

Katika shule yetu tuna mabasi matatu ambayo hutumiwa kuwapeleka nyumbani na kuwarudisha watoto/wanafunzi shuleni, kutupeleka safari pamoja na vitu vingi. Tuna madereva watatu na kila mwalimu anastahili kuwa anajua kuendesha gari.

Ninaipenda sana shule yangu kwani haina ukabila kwasababu kuna wanafunzi wengi ambao ni wa makabila tofauti.

## MASWALI

i) Shule ya mwandishi inapatikana wapi? (Alama 01)

ii) Taja idadi ya wanafunzi katika shule hii (Alama 02)

iii) Taja mataifa ambayo baadhi ya wanafunzi katika shule hii hutoka.(Alama 03)

iv) Wanafunzi katika shule hii hufanya nini jumapili mchana? (Alama 03)

## Soma habari ifuatayo na ujibu maswali hapo chini;

**KUCHANJWA**

Wizari ya afya ina jukumu kubwa la kuchanjwa kwa Watoto. Hii ni kwa sababu inaamini ya kuwa kukinga magonjwa ni bora kuliko kuyatibu. Kwa hivyo, kinga ni bora kuliko tiba. Vilevile, wazee wetu walisema 'tahadhari kabla ya hatari'. Watoto nao ni wepesi mno kupata magonjwa hasa yale ya kuambukiza. Hii ndiyo maana tunaona wizara ya afya ikitoa huduma hizi za chanjo hospitalini na katika zahanati. Watoto hawa ambao ni viongozi wa kesho wasipate kuugua ugonjwa kama vile Pepo punda, kifaduro, kifua kikuu, polio, ndui na surua. Haya yanawezekana kwa chanjo, kupiga sindano na kumeza dawa kwa kufuata ratiba ya chanjo ifuatayo;

| Kabla ya mtoto kuzaliwa | Mtoto anapozaliwa | Akiwa mwezi mmoja | Akiwa miezi miwili | Akiwa miezi mitatu | Akiwa miezi tisa | Ak iw a mwaka mmoja na nusu | Aki anz a kw end a shu len i |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ma m a Mja Mzito Atapigwa Sindano Ya kuzuia Pepo Punda Mara moja au mbili | **Kifua kikuu** (Sindano) | **Pepo punda** **Kifaduro** (sidano) **Ndui** (chanjo ) **Polio** (kumeza dawa) | **Pepo Punda** **Kifaduro** **Polio** **(**chanjo) | **pepo punda** **Kifaduro** **polio** | **Surua** (sidano) | **Pepo punda** **Kifaduro** **polio** | **Pepo punda** **Kifaduro** **Polio** **kifua kikuu** **ndui** |

**Maswali;**

1) Tafsiri magonjwa kwa kiingereza; **Pepo punda(Tetanus), kifaduro (whooping cough),kifua kikuu (Tuberculosis), Surua (Measles) Ndui (Small pox) Polio(Polio)**
2) Ni wizara gani inayofanya kazi ya chanjo za Watoto?..................................
3) Kwa nini wizara hii inafanya kazi ya kuchanjwa kwa mtoto?................................
4) Watoto ni rahisi kushikwa na maradhi au ugonjwa gani?.....................................
5) Taja magonjwa haya yanayokingwa Watoto........................................................
6) Magonjwa haya yanakingwa kwa njia gani?.....................................................
7) Kwa kufuata ratiba ya chanjo, mtoto hupewa kinga ya pepo punda kwa mara ngapi?
8) Sidano ya kifaduro hupigwa mara ngapi?................................................
9) Ni ugonjwa gani ambao hukingwa kwa mara chache sana?...............................
10) Taja ugonjwa ambao hukingwa kwa mara nyingi?...........................................

10.Wewe kama mtoto, wazazi wako wamewahi kukupeleka hospitalini kuchanjwa?

11. Ulipata chanjo kutoka hospitali gani?...........................................

12. Ni ugonjwa gani unaokusumbua katika maisha yako ya sasa?....................

1. **Soma kifungu cha habari hiki kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini;-**

## MATATIZO NI SEHEMU MOJA YA MAISHA;-

Bibilia tukufu inasema kwamba Mungu alimuumba binadamu katika picha yake halisi. Inaaminika kuwa Mtu ambaye Mungu alimuumba kwanza ni Adamu. Na baada ya kuona kwamba Adamu alikuwa na upweke mwingi bila ya furaha, Mungu aliamua kumuumba Hawa ili aweze kumfariji na kumfurahisha katika maisha yake. Aliwapa maskani bora katika shamba la Edeni. Adamu na Hawa walikuwa na furaha tele maishani mwao kwenye shamba hilo. Lakini baada ya kufanya maovu na kumkosea muumba wao, Mwenyezi Mungu alikasilika sana akawalaani na kuwafukuza wote watoke kwenye shamba lake tukufu. Tangu siku hiyo, kila mwanadamu alilaaniwa na Mungu. Na hii ndiyo maana kuna matatizo na <u>changamoto chungu nzima</u> zinazomfuata binadamu kila usiku na mchana.

Tangu kuumbwa na kuzaliwa kwake, mwanadamu hupata mateso kadhaa na kumsababishia ugumu wa maisha. Zamani zile <u>maisha yalikuwa matamu mithili</u>

ya asali ilhali maisha ya siku hizi ni machungu kama shubiri. Hii ndiyo sababu mwafaka inayoelezea kwanini watoto wachanga wanalia sana punde tu baada ya kutoka kwenye matumbo ya akina mama - wazazi wao. Wataalam wengi, yaani wajuzi wa mambo, wanasayansi pamoja na wanafalsafa wanasema kwamba mazingira mapya ndiyo yanayowasababishia watoto hawa wachanga kulia kwi!kwi!kwi! . Hata uzazi wenyewe ni mgumu. Lakini nilipowauuliza swali hilo mababu zangu wawili yaani; Mzee Bakidawo Kisitu na Jaajja Lujja Muteeweta, walinijibu kwamba; "watoto wachanga hawa wanalia kwa sababu huwa wameogopa matatizo na changamoto wanazozitegemea kuzipata hapa katika dunia au mazingira mapya"

Kila wakati, saa na dakika kuna mwanadamu anayekabiliwa au anayekumbwa na hali ngumu ya maisha. Dunia ni kigeugeu kama kinyonga au lumbwi! Dunia imebadilika sana na kila mabadiliko yanamuathiri mtu fulani . Miongoni mwa matatizo na changamoto kubwa wanazozipata wanadamu maishani mwao ni kama vile;-

Ugonjwa, kuna magonjwa sugu mbalimbali yanayotishia usalama na kushambulia afya ya binadamu na hatimaye kusababisha kifo; kama;- UKIMWI , Ebola, homa ya Malaria , nakadhalika..

Umaskini ni changamoto nyingine kubwa kwa binadamu. Maskini ni yule mtu duni ambaye hana uwezo wa kukidhi mahitaji yake msingi maishani. Asiye na mbele wala nyuma, hohe hahe!. Umaskini unatokana na mambo kadha wa kadha kama vile ; uzembe na uvivu, ukosefu wa ajira, Pamoja na ujinga wa mtu binafsi.

Njaa ni tatizo lingine kwa binadamu. Njaa ni ile hali ya ukosefu wa chakula cha kutosha. Maisha ya binadamu yanategemea chakula na bila ya chakula binadamu hawezi kuishi. Siku hizi kupata riziki au chakula ni vigumu hapa duniani kama kukwea mlima Kilimanjaro au Rwenzori. Na watu wengi wamekufa kwa sababu ya njaa. Uhaba ama ukosefu wa chakula mara nyingi husababishwa na mambo tele kama vile; ukame au uhaba wa mvua, udongo au ardhi isiyo na rutuba ya kuiwezesha mimea kukua vizuri, majanga makubwa kwa mfano dhoruba, ghalika

au mafuriko( mvua nyingi) yanasababisha uharibifu mkubwa wa mashamba, mali pamoja na vifo vya watu.

Migogoro katika jamii ni changamoto nyingine. Hapa tunaona kwamba mwanadamu anapata na kupitia migogoro chungu nzima. Kama vile;- kugombana, kupigana, kurogana na kuuana. Vita vya wenyewe kwa wenyewe katika dunia hii vimesababisha vifo vya wanadamu wengi, kusambaratika kwa familia, ongezeko kubwa la wakimbizi, ukosefu wa usalama au amani na mdororo wa kiuchumi. Kwa mfano, hapa nchini Uganda kumekuwa na vita mbalimbali kwa mfano; vita vya kikundi cha waasi LRA wanaongozwa na Joseph Konny kule kaskazini mwa Uganda. Wananchi wengi huko wilayani Gulu,kitgum,Lira, Moyo, Pakwach nakadhalika, walipoteza mali pamoja na uhai wao vitani.

Mfano mwingine ni nchi ya Rwanda ambapo kulitokea vita vikali sana baina ya Wahutu na Watutsi. Marafiki , ndugu na majirani wote waliuana kwa sababu ya ukabira. Maelfu na maelfu ya watu walifariki dunia katika mauaji ya halaiki yaliyotokea nchini humo. Mfano wa pili ni nchi ya Kongo. Katika Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo, watu wengi wamehama makazi au nyumbani kwao na kukimbilia usalama wao katika nchi jirani na wengine wameuawa vitani.

Kwa hivyo, kila mwanadamu anapitia mambo na matatizo au changamoto mbalimbali katika kukua kwake toka utotoni hadi ukubwani.

Hali na mfumo huo wa maisha utaendelea daima dawamu ama milele na milele. Tunamwomba Muumba Mwenyezi Mungu Mola Subhana Rabuka Allah aturehemu sana na kutusamehe madhambi yetu. Ameni.

**Maswali;-**

a) Pendekeza mada nyingine iliyo mwafaka kwa habari hii.
b) Mungu alimuumba mtu gani mwanzoni?
c) Mungu alikasilishwaje hadi akawafukuza Adamu na Hawa shambani Edeni?
d) Kulingana Bibilia, eleza sababu kwa nini binadamu anapata matatizo maishani mwake?
e) Kwa nini watoto wachanga wanalia wanapozaliwa?

f) Taja na uelezee mbinu au fani za lugha alizozitumia mwandishi katika habari hiyo.

g) Binadamu anakabiliwa na changamoto gani hapa duniani?

h) Eleza madhara ya vita vya wenyewe kwa wenyewe katika jamii.

i) Eleza maana ya vifungu vya maneno vifuatavyo;-

   i) changamoto chungu nzima.
   ii) Dunia kigeugeu
   iii) Asiye na mbele wala nyuma.
   iv) Maisha yalikuwa tamu mithili ya asali.
   v) Mauaji ya halaiki.

(i)**Tuvae Mavazi ya heshima**

Sisi wanadamu hatuendi uchi kama wanyama.Sisi huvuaa nguo,viatu,kofia,vilemba na mapambo mengineyo kama kila moja

wetu apendavyo .Mavazi yana muhimu mkubwa katika maisha yetu.Kwanza,mavazi hutusaidia kujikinga dhidi ya baridi au joto. Pili,mavazi hutusaidia kuficha sehemu nyingi za siri kwenye mili yetu.

Lakini siku hizi,vijana wengu hasa wasichaaa huvaa mavazi ambayo si ya heshima.wasichana wengu siku hizi atawakuta makivaa mavazi ambayo pamoja na kuwambana sana na hata yanaweza kuonyesha sehemu zao za siri za juu ya magoti.Baadhi ya wasichana huvaa nguo ambazo zinawesesha macho kupenyeza ndani yake na kuangalia mavazi ya ndani kama vile chupi au sidiria . Hata hivyo,wasichana wengine huvaa nguo ambazo zichanaa sehemu za migongo yao wazi kabisa . Mavazi kama haya ambayo yanaonyesha maumbile wazi wazi pamoja na sehemu za siri si ya hashima kulingana na utamaduni wa kiafrika.Jambo la kushangaza ni kwamba baadhi ya wana wake nao huvaa vivyo.Unamkuta mkwe wa bwana Fulani amevaa rinda ambalo pamoja na kumbana ,ni fupi sana.Hata akiwa anatembea ,mapaja yanaonekana wazi wazi huku matako yaliyobanwa na rinda hilo.yakibenukabenuka na kuonyesha pindo za chupi aliyovalia ndani ya rinda .

Kulitokea kisa kimoja kanisani cha kuaibisha sana .Msichana mmoja alikwenda kuhudhuria ibada ya jumapili huku amevaa rinda fupi sana na

lenye kumbana barabara .Msichana huyo ambaye alikuwa mwanafunzi katika shule Fulani ya upili alifika baada ya ibada kuanza na hiyoiyeey akakaa kwenye viti vya nyuma.

Ibada hiyo ilikuwa maalum kwa sababu waliohudhuria waliombwa kushiriki katika ile sakramenti ya kukumbuka kufa Bwana Yesu Kristo.Na kwa hiyo aliwabidi waumini kwenda polepole kwenye altare na kupiga magoti mbele ya kasisi.Basi ,walikalia viti vya mbele ndio waliotangulia wakafuatiwa na wale wa wa viti vya katikati na mwishowe wale wa viti vya nyuma.

Zamu ya msichana huyo ilipofika ,yeye bila aibu yoyote akasimama na kwenda mbele kwenye altare ili apate ile sakramenti takatifu.Msichana huyo alipokuwa akipita katikati akielekea kwenye altare ,waumini wote walishanga sana kwa vile alivyokuwa amevaa nguo ya aibu hadharani .Rinda lilikuwa fupi sana kiasi kwamba mapaja ya msichana huyo yalikuwa yanaoneka wazi kabisa .Isitoshe hiyo ,rinda lake msichana huyo lilikuwa linambana sana hata alikuwa na matatizo kwa kutembea.Alikuwa akitembea .Alikuwa akitembea mfano wa mfungwa au mwendawazimu aliyefungwa kwa pingu miguuni.

Haya basi ,msichana akafika kwenye atare akajaribu kupiga magoti lakini akapata taabu.Akajaribujaribu na mwishowe akafaulu kupiga magoti likini kwa shida sana.

Lakini alipokuwa akingonja ili kasisi aje ampe kipande cha mkate pamoja na Mvinyo kama ilivyo kawaida ya sakramenti hiyo,waumini nyuma yake wakaanza kupiga makelele wakinungunika.

Wengine wakasema ,"Hapana, asipewe mkate na mvinyo!Hastahili hivyo.Yeye amekosa abadu."

Hata wanawake nao wakasema,"Hapana!Mavazi haya ya kisasa  sasa yamevuka mpaka na kugeuka kitu kingine .Mbona yeye ameaibisha jamili ya wanawake"

Watoto ambao wao hawakujua ni aibu gani msichana alirusha,walikuwa wanacheta tu kwa  kuwa wanachungulia chupi ya msichana huyo wakati alipokuwa akipga magoti.

Je, aibu gani iliyotokea,mpaka waumi wakapata kunungu’unika hivyo ? Ndugu yangu ,maajabu kweli yalitokea !Msichana Yule alipopiga magoti,rinda lake likaenda juu zaidi na kuacha matako yake wazi isipokuwa chupi aliyoivalia ndani.Ikawa aibu kubwa na mwanamume mmoja akasimama akamwendea Yule msichana akamkamata mkono akamvuta nje.Msichana alikuwa bado hajapewa bado hajapewa mkate na mvinyo.Kisa hicho kweli kiliiharibu ibada hiyo takatifu.Ndugu yangu ,ingawa tuna haki ya kuvaa kama vile tupendavyo,inatupasa kupasa kupasa kujiheshimu na kuvaa mavazi yenye heshima .Tuheshimu utamaduni wetu wa kiafrika ambao hauungi mkono mavazi yanayoonyesha sehemu za siri za mwili.Lazima tuvae mavazi ya heshima ,nasi tuwe na heshima.

**Jibu Maswali Yafuatayo**

1.Toa sababu tatu muhimu ukielezea umuhimu wa mavazi kwa binadamu.

2.Je,mavazi ambayo yanachukuliwa kama si ya heshma ni mavazi ya aina gani?

3.Fanyu utafiti na uandike sehemu zote za mwili wa binadamu.

4.Msichana anayezungumiziwa katika taarifa hii alikuwa amevaa vipi?

5.Kwa nini msichana huyo alikalia kwenye viti vya nyuma msichana alipopiga magoti kwenye altare?

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini;**

Muziki ni burudani muhimu kwa binadamu hapa duniani. Kwa kweli Kuna waimbaji au wanamziki wengi sana katika nchi tano za Jumuiya ya Afrika mashariki. Wanamziki hawa wameimba nyimbo nzuri nyingi mwaka huu na ni vigumu sana kuamua au kuchagua wimbo mzuri zaidi ya nyimbo zote zilizozinduliwa mwaka uliopita. Kuna waimbaji wakubwa na waimbaji wadogo. Miongoni mwa waimbaji Watano wakubwa sana hapa Afrika mashariki mwaka uliopita kuna; Jose Chameleon, Diamond Platinumz, Sauti Sol, Bebe Cool na Eddy Kenzo. Waimbaji hawa wana nyimbo Chungu nzima. Nyimbo zao zote zinaburudisha, zinaelimisha na kufurahisha watu katika jamii. Mwimbaji mwenye nyimbo nyingi zaidi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni Bebe Cool. Ana nyimbo zaidi ya mia moja (100).

Mwimbaji maarufu sana nchini Tanzania na ni Diamond Platinumz. Nyimbo zake zinavuma sana hapa Afrika Mashariki na duniani kote. Fundi mitambo wa Diamond Platinumz anaitwa Master Jay na anasema kwamba Diamond ana nyimbo zaidi ya 50.

Watu wengi wanaenda kwenye matamasha, Kilabu na diskoni usiku kwa sababu wanataka kusikiliza na kucheza muziki mzuri wa waimbaji hao. Vijana wa siku hizi wavulana kwa wasichana wanajua kucheza muziki vizuri. Wasichana wanatingisha matiti na matako yao pamoja na sehemu nyingine za mwili. Wavulana wanarukaruka juu na chini huku wakichanganya miguu yao. Lakini kati ya wavulana na wasichana ni nani wanaojua kucheza vizuri zaidi? Muziki ni mzuri kwa kila mtu hata wakiwa watoto wadogo, vijana, wakubwa na wazee. Kwa kweli,Watu wote wanapenda muziki duniani. Wazee wengi wanataka sana kusikiliza muziki wa zamani, yaani ule muziki wa enzi zao . Baadhi ya wazee wanapendelea sana muziki mwororo wenye mwendo wa polepole.

Ninaitwa Mukungu Collins. Mimi ni mvulana mwenye umri wa miaka kumi na Sita. Mimi ni mwananchi wa Uganda. Ninaishi mjini Kawempe, kaskazini mwa jiji la kampala. Mimi kama kijana wa kizazi kipya ninapendealea zaidi mziki wa Kijamaica maishani mwangu. Kuna waimbaji wakubwa wa kijamaica kama vile; Konshens, Busy Signal, Nicki Minaj, Bennie Man, Mr.Vegas, Patra, Tiana, Shaggy, Alaine, Kartel na Gyptian. Ni kweli kwamba Wajamaica wanaimba vizuri muziki wao wa aina ya reggae , ragga na dance hall.

Lakini mimi kama mpenda mziki, ninaona kwamba Wimbo mzuri wa mwaka uliopita ulikuwa ‘Kutama’*!* Wimbo huo umeimbwa na Fik Fameika. Mbali na wimbo huo, Mwanamziki huyo Fik Fameika ana nyimbo nyingine nyingi nzuri. Kwa mfano; Mbega wa baala, Gwe abisobola, Kachima, Mafia, Movie, Somebody, Mutuwulira, Property, Pistol , nakadhalika…

Hapa shuleni ninao Marafiki wengi sana ambao wanapenda mziki kama mimi. Wengi wao ninasoma nao Kiswahili katika kidato cha tatu. Miongoni mwa marafiki hawa ni; Twebaze, Agaba, Adinani, Bashir, Mutoni , Bukenya na katusiime . Tunapendana mno kama mlevi na pombe. Wanafunzi hao wanajua kuimba nyimbo na kucheza mziki wa kila aina. Tunacheza pamoja kwenye kikundi cha Nato katika Kilabu ya EAC. Wanajua kucheza Lingala, Hip-hop, B-Boy, Dance hall, RnB, nakadhalika..

***Maswali;..***

(a) Mwandishi wa habari hiyo ni nani? Je, ni mwananchi wa nchi gani?.

……………………………………………………………………………..

..........................................................................................................

(b) Mwandishi ana umri wa miaka mingapi? Anasoma kidato cha ngapi?

…………………………………………………………………………………

..........................................................................................................

(c) Mwandishi anapendelea zaidi muziki wa aina gani?

……………………………………………………………………………….

(d) .Wazee wanapendelea sana kusikiliza na kucheza muziki wa aina gani?

…………………………………………………………………………………

(e) Mwandishi pamoja na familia yake wanaishi wapi?

…………………………………………………………………………………..

f) Andika majina ya waimbaji wakubwa sana Afrika mashariki.

1……………………… 2………………………… 3…………………….

4………………………… 5…………………….

g) NI nani Mwimbaji mkubwa wa mwaka elfu mbili kumi na saba? Aliimba wimbo gani?

…………………………………………………………………………………..

h) Toa umuhimu wa muziki kwa watu katika jamii.

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

i) Wewe kama mtoto wa kizazi kipya, unataka kucheza muziki wa aina gani?

.........................................................................................................

j) Andika majina manne ya wanamuziki wako wakubwa wa kijamaica.

1......................... 2......................... 3...................... 4..................

k) i) Ni mwimbaji gani maarufu anayevuma sana nchini Tanzania?

................................................................................................................

ii)Je, ana jumla ya nyimbo ngapi?

1. **Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini.**

Ivy ni mwananchi wa Uganda. Ni mschana mwenye umri wa miaka kumi na sita. Anaishi katika wilaya ya Nakaseke pamoja na wazazi wake.Wazazi wa msichana huyu ni wafanyabiashara na wanapata pesa nyingi kutokana na kazi yao hiyo. Wana maduka Matatu hapa jijini kampala. Wanauza bidhaa kama vile; viatu na Nguo za wanaume na wanawake, mikoba katika duka lao la kwanza , Viatu vya wanawake na wanaume –wadogo na wakubwa. Kwenye duka lingine wanauza simu na vyombo mbalimbali vya simu, Duka lao la tatu ni la kompyuta na vifaa vyake nakadhalika. Pesa takribani zote wanazozipata wanazilipa shuleni kama karo ili binti yao Ivy asome.

Huyu mtoto wa kike Ivy ndiye kifungua mimba katika familia ya Bwana Mukiri na Bi. Nakazzi. wazazi wote wawili, yaani baba na mama yake wanampenda sana mtoto wao si kwa sababu ya kuwa wa kwanza kuzaliwa katika familia yao tu, bali pia ni kwa sababu ni mwerevu sana masomoni. Kila muhula na kila mwaka, yeye ndiye anachukua nafasi ya kwanza na kuwaongoza wengine darasani.Ivy ni mwanafunzi katika shule ya upili ya Nakaseeta na anasomea katika kidato cha tatu.

Mwaka uliopita, aliwashinda wanafunzi wote wa kidato cha pili. Waswahili walisema kweli kwamba akili ni mali na hawakukosea kwa sababu Ivy alipewa zawadi chungu nzima kutoka kwa mkurugenzi wa shule,walimu, wazazi na marafiki zake. Lakini zawadi ambayo kwa kweli ilikuwa kubwa sana kuliko zote alizozipata siku hiyo ni udhamini. Ivy alipewa nafasi ya kusomea bure mpaka atakapomalizia masomo yake ya sekondari katika shule yake hiyo ya Nakaseeta. Shule ya Ivy iliamua kuchukua jukumu la kumdhamini na kugharamia masomo yake baada ya kuona na kuhakikisha kwamba msichana huyu anapenda sana kusoma na ni mwenye bidii masomoni. Isitoshe, kila kitu anachokifanya, anakifanya kwa nguvu na moyo mmoja. kwa mfano; kucheza michezo kiwanjani, kuimba kwenye kwaya ya shule na kulima shambani. Baba na mamake Ivy, yaani Mzee Mukiri na Bi.Nakazzi wote wanasema kwamba mtoto wao Ivy amekuwa mwerevu sana tangu utotoni mpaka sasa ukubwani hajabadilika hata kidogo.

Walimu wote ambao waliwahi kumfundisha Ivy darasani, wanasema kwamba ndiye mwanafunzi pekee anayeweza kukwangula alama takribani zote, na wakati mwingine hupata asilimia mia moja katika mitihani na mazoezi. Mwalimu wake wa somo la Kiswahili bwana Kisitu Samuel naye anasema ,“Ivy ni mwanafunzi mwerevu na hodari masomoni na anapendelea sana somo la lugha ya Kiswahili”

***Maswali;***

a. Ivy ni mwananchi wa nchi gani?

……………………………....................................………………

b. Wazazi wake Ivy wanaishi katika wilaya gani?

……………………………….........................................………

c. Andika machache Kuhusu wazazi wa Ivy.

.......................................................................................................

d. Kwa nini walimu na walimu walimpenda sana Ivy ?

..............................................................................................

e. Wazazi wake Ivy wanafanya kazi gani?

..........................................................................................

……………………………………………………………………………………

f. Ivy anasomea katika shule gani? Na anasoma katika kadato cha ngapi?

..............................................................................................

g. Toa sababu kwanini shule ya Ivy inadhamini masomo yake?

………………………………..........................................................................

……………………………………………………………………………………

h. Taja mambo mawili mazuri ambayo Ivy anayafanya.

.............................................................................................

……………………………………………………………………………………

i. Pendekeza mada mwafaka kwa habari hiyo.

……………………………………………………………………………………

j. Kwa nini wazazi na walimu wa Ivy wanampenda sana?

..............................................................................................

**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini;.**

Karibu na kijiji maarufu cha Nimirokukabala- wilayani Nakaseke, paliishi mwanamume mmoja aliyejulikana kwa jina Bwana Mudiribada Zephaniah. Na mke wake alikuwa akiitwa Bibi Musama Suzana. Familia hii haikuwa maskini wala tajiri.Ilikuwa ya wastani kiuchumi. Hata hivyo, walikuwa hawaazimwi nguo, hawaombi sukari wala chumvi kwa majirani yao. katika familia hii kulikuwa na watoto kumi . wasichana wakiwa watatu na wavulana saba. Kifungua mimba yaani mtoto wa kwanza kuzaliwa katika familia hii alikuwa ni msichana ilhali kitinda mimba ni mvulana. Watoto hawa walikua vizuri wakiwa wazima wa afya.

Bwana Mudiribada alikuwa mkulima maarufu sana. Mwaka wa 1995, Mudiribada ndiye aliyeshinda wakulima wote katika wilaya nzima ya Nakaseke. Shamba lake kubwa lilikuwa limejaa mimea ya aina mbalimbali na mifugo. Alikuwa na wafanyakazi chungu nzima ambao walimsaidia sana katika kazi nyingi pale shambani. Familia nzima; yaani baba, mama na watoto walikuwa wakiamka asubuhi na mapema kwenda kufanya kazi za shambani kila siku, isipokuwa Jumapili tu. Siku ya Jumapili ilikuwa siku ya kuenda kuhudhuria maombi kanisani.Watu takribani wote katika familia hii walikuwa wachamungu. Kwa hivyo, kwa mtu mchamungu ni vigumu sana kukosa maombi kanisani siku ya Jumapili. Watoto watatu walikuwa waimbaji katika kwaya ya kanisa.

Kuna shughuli nyingi sana ambazo Bw.Mudiribada alihakikisha kwamba zinafanywa ndani ya wakati ili shamba lake liweze kulete faida kubwa. Kazi ya kwanza ni kufyeka na kulima konde au shamba. Magugu yanalimwa na kung’olewa, nyasi zinakusanywa na kuchomwa moto. Kazi ya pili ni kupanda. Kupanda ni kitendo cha kuweka mbegu ardhini ili ziote. Baada ya siku chache, mbegu zinaanza kuota kutoka ardhini. Kazi ya tatu ni kupalilia. Kupalilia ni kitendo cha kulima na kung’oa magugu na nyasi ili mimea iweze kukua vizuri, kuchanua vizuri na kuzaa matunda na chakula. Kazi ya nne ni kumwagilia. Umwagiliaji ni kitendo cha kunyunyuzia mimea maji ili mimea hiyo iwe na maji ya kutosha ya kuiwezesha kukua vizuri.

Pia kuna kazi ya tano ya kunyunyuzia dawa na mbelea kwenye mimea. kazi ya kunyunyuzia mbolea pamoja na dawa ya kupiga vita wadudu na ugonjwa wa mimea. Mimea yenye kinga ya dawa na mbolea inakua vizuri na kunawiri.  Kazi ya sita ni kuvuna. Baada ya matunda au chakula kwenye mimea kukomaa vizuri, wafanyakazi wanavuna chakula ama matunda au mazao hayo na kuyatoa shambani. Kila baada ya mazao kuvunwa shambani, mazao kama vile; mahindi, maharagwe, mtama na wimbi; yalikuwa yakipelekwa nyumbani na kuwekwa au kuhifadhiwa kwenye ghala. Mazao mengine kama vile; matunda na mboga yalikuwa yakipelekwa sokoni kuuzwa kabla ya kuharibika. Mazao mengine kama vile; Pamba, kahawa, ngano na mchele; yanaweza kuchukuliwa kuuzwa viwandani kama malighafi baada ya kuyakausha vizuri ili kutengenezea chakula, bidhaa na vifaa mbalimbali.

Kwa hivyo, Bw.Mudiribada alikuwa anaingiza pesa nyingi baada ya kuuza mazao yake sokoni.Pia alikuwa anapata chakula cha kutosha kulisha familia yake nzima.

***Maswali;***

a) kulingana na habari, ni nani mkuu wa familia katika hadithi?

b) Kifungua na kifunga mimba wa Bw.Mudiribada walikuwa watoto gani?

c) Eleza kazi sita ambazo Bw.Mudiribada alihakikisha kwamba zinafanywa vizuri ndani ya wakati ufaao hapo kwenye shamba lake.

d) Bw.Mudiribada hakuwa mtu maskini wala tajiri sana. Unadhani ni kwa sababu gani?

e) Familia ya mwandishi ilikuwa inapatikana wapi nchini Uganda?

f) Umaarufu wa Bw.Mudiribada Zephaniah ulitokana na kazi gani haswa?

g) Bw.Mudiribada alipata mafanikio gani katika mwaka wa 1995?

h) Pendekeza mada au kichwa cha habari kilicho mwafaka kwa habari hiyo.

i) Kwa nini mwandishi wa habari anasema kwamba familia ya Bw.Mudiribada ilikuwa ya watu Wachamungu? Toa sababu mbili.

j) Baada ya Bwana Mudiribada kuvuna mazao yake shambani, mazao hayo yalikuwa yakichukuliwa sehemu mbalimbali. Andika majina ya mazao;-

i. Yaliyohifadhiwa kwenye ghala;

ii. Yaliyokuwa yakipelekwa sokoni;

iii. Yaliyokuwa yakipelekwa viwandani kama malighafi ya kutengenezea bidhaa;

## ZOEZI

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini.**

RAFIKI YANGU MPENDWA.

Rafiki wa kweli ni mtu anayekusaidia wakati wa shida na furaha. Mwanadamu ambaye si rafiki anakula na anakuwa nawe wakati wa furaha pekee na atakukimbia na kukuacha wakati wa shida. Mtu anayekataa kukusaidia wakati wa shida si rafiki. Mtu wa aina hiyo ni adui kabisa. Katika hii dunia ya Mungu kuna marafiki na maadui.

Ninaitwa Mutabali Hamza. Mimi ni kijana mwenye umri wa miaka kumi na sita. Mpaka sasa hivi ningali mwanafunzi. Ninasoma kidato cha pili. Nyumbani kwetu ni Tororo. Wazazi wangu wanaishi mjini Tororo, upande wa mashariki mwa Uganda. Nina marafiki wengi sana katika shule yangu na nyumbani kwetu. Nina marafiki wa kike wanne na marafiki wa kiume watano tu. Marafiki wa kiume ni; Kalyesubula, Bosiko, Mukisa, Kataala na Kadingo. Marafiki yangu wa kike ni; Namugenyi, Kisakye, Nakigozi na Teta. Marafiki hawa wote ninawapenda sana kwa sababu wananipenda pia.

Miongoni mwa marafiki wote, ninampenda sana Bosiko. Bosiko ni rafiki yangu wa dhati. Bosiko ninampenda sana kwa sababu yeye ni mtu mzuri. Bosiko ana tabia nzuri. Ni msafi. Anafua yunifomu yake na kuipiga pasi vizuri, anavaa viatu na soksi kila siku. Anafagia darasa na kupiga deki. Bosiko ana mwandiko mzuri katika madaftari yake. Anasoma kwa bidii na ni mwerevu na mjanja kama Sungura. Kila kitu tunagawana. Hata chakula, chapatti, samosa tunakula pamoja. Sabuni, sukari, mavazi, kalamu tunatumia pamoja.

Vvule Nago aliiba pesa zangu lakini Bosiko alinipatia pesa zake. Bosiko ni mtu mwenye huruma. Ni mhisani na msamalia mwema. Bosiko anaenda kanisani kila Jumapili. Kila siku anapiga magoti na kuomba Mungu. Bosiko ni mchamungu wa kweli. Kila mwaka, Bosiko anakuwa nambari moja darasani. Anasoma vitabu vyake kwa bidii. Walimu wetu wote wanampenda mno kwa sababu ni mwanafunzi mwenye tabia nzuri shuleni.
Ninaomba Mwenyezi Mungu atubariki sana tuwe marafiki wa kweli, tupendane kwa dhati milele na milele.

***Maswali;***

(a) Ni nani rafiki wa kweli?.

……………………………………………………………………………………….

(b) Ni nani rafiki ambaye si wa kweli?.

……………………………………………………………………………………….

(c) Andika jina la mwandishi wa habari hiyo

……………………………………………………………………………………..
(d) Mwandishi ana umri wa miaka mingapi?

…………………………………………………………………………………….
(e) Mwandishi anasoma kidato cha ngapi?

……………………………………………………………………………………
(f) Wazazi wa mwandishi wanaishi wapi?

……………………………………………………………………………………..
(g) Mwandishi ana Marafiki wa kike wangapi?.

………………………………………………………………………………………
(h) Andika majina ya marafiki wa kike wa mwandishi?

………………, ……………………, …………………………, …………..
(i) Marafiki wa kiume wa mwandishi wako wangapi hapo shuleni?.

……………………………………………………………………………….
(j) Taja majina ya marafiki wa kiume wa mwandishi.

……………………………………………………………………................
k) Mwandishi ana rafiki wa dhati. Ni nani huyo?

………………………………………………………………………..
l) Kwanini Mutabali anampenda sana Bosiko? Andika sababu tano;

i). …………………………………………………………………………

ii) …………………………………………………………………………

iii) …………………………………………………………………………

iv)…………………………………………………………………………

v) …………………………………………………………………………..
m) Kwanini Walimu wote wanampenda sana Bosiko? Toa sababu.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………

## SEHEMU B

2. **Andika sentensi zifuatazo katika Wingi;** *(Alama 10)*

| | UMOJA: | WINGI: |
|---|---|---|
| a) | Sitaki kula chakula | |
| b) | Huu ni mlingoti mlimani | |
| c) | Huyu ni mke wangu. | |
| d) | Wewe huli nyama. | |
| e) | Gari haliondoki sasa. | |

3. **Andika sentensi Tano ukitumia vivumishi vifuatavyo;-** ***(Alama 05)***

   a) (Hatari)…………………………………………………………………

   b) (Rahisi)…………………………………………………………………….

   c) (Bora)……………………………………………………………………..

   d) (Kisasa)……………………………………………………………………

   e) (-embamba)…………………………………………………………………

4. **Jaza mapengo kwenye jedwali**. ***(Alama 10)***

| HALI YA KUKUBALI | HALI YA KUKANUSHA;- |
|---|---|
| 1. Ninasoma kitabu | ……….. |
| 2. Tulifanya kazi. | ……………. |
| 3. Unaandika barua | …………….. |
| 4. ………… | …………… |
| 5. …… | Sitafagia vumbi darasani |

5. **Andika sentensi Tano ukitumia kivumishi cha pekee '–o-ote'** ;- *(Alama 05)*

   a) ……………………………………………………………

b) ……………………………………………………………………

c) ……………………………………………………………………

d) ……………………………………………………………………

e) ……………………………………………………………………

**6. Andika sentensi Tano katika wakati uliopita hali Timilifu, kwenye hali ya kukanusha;-** *(Alama 10)*

a) ……………………………………………………………………

b) ……………………………………………………………………

c) ……………………………………………………………………

d) ……………………………………………………………………

e) ……………………………………………………………………

**7. Jaza sentensi katika jedwali lifuatalo;** ***(Alama 30)***

| **Wakati uliopo.** | **Wakati uliopita** | **Wakati ujao.** | **Wakati uliopo hali Timilifu** |
|---|---|---|---|
| **1. Sili chakula.** | | | |
| **2…** | **Musa hakusali** | | |
| **3.** | | **Tunda halitaiva.** | |
| **4.** | | | **Maji hayajafika.** |
| | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **5. Hulali usiku** | | | |
| **6.** | **Simu hakuibiwa** | | |
| **7.** | | **Kioo kitapasuka** | |
| **8..** | | | **Mkeka umeloa maji.** |
| **9. Moto unawaka** | | | |
| **10.** | **Niliota ndoto usiku** | | |

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yaliyo hapo chini yake;**

Mtu yeyote hapa duniani ana kitu anachokipenda zaidi ndani ya moyo wake. Mimi ninapenda muziki kwa moyo wangu wote. Watu wote wanaume kwa wanawake wanapenda muziki. Muziki ni burudani ya maana sana katika maisha ya mwanadamu. Kuna umuhimu mwingi wa muziki katika jamii yetu. Kwa mfano; Muziki huburudisha watu katika jamii – wanaimba na kucheza muziki kwa furaha kwenye matamasha na diskoni. Muziki unapatia watu kazi au ajira na wanamuziki wanapata pesa nyingi kutokana na kazi yao ya kucheza na kuimba nyimbo. Pia muziki ni chanzo cha furaha na ni faraja kwa watu wenye shida, mawazo, huzuni na matatizo mengine ya dunia. Muziki pia ni chanzo cha mapato ya nchi. Nchi nyingi kama vile Jamaica wanaingiza pesa nyingi za kigeni kutokana na muziki wao. Muziki hufundisha tabia nzuri kwa watu katika jamii. Muziki hukuza na kusambaza lugha husika katika jamii; Kwa mfano Kiswahili kuna waimbaji au wanamuziki wanaoimba nyimbo zao kwa kutumia lugha yetu nzuri ya Kiswahili.

Pia muziki ni chanzo cha umaarufu au kujulikana kwa watu hawa wanamuziki katika jamii zetu. Waimbaji karibu wote tunapata kuwajua kupitia nyimbo zao wanazoimba. Kwa mfano hapa nchini Uganda kuna

mtoto maarufu sana anaitwa Fresh Kid. Fresh Kid ni mwimbaji mpya mwenye umri wa miaka Saba tu. Anaimba nyimbo za miondoko ya kisasa zenye mtindo wa Hip-hop. Dunia nzima imepata kumjua mvulana huyu Fresh Kid kwa sababu anaimba vizuri. Kwa hivyo, umaarufu wa Fresh Kid umetokana na muziki wake.

Hapa katika nchi za jumuiya ya Afrika mashariki. Wanamziki hawa wameimba nyimbo nzuri nyingi mwaka huu na ni vigumu sana kuamua au kuchagua wimbo mzuri zaidi ya nyimbo zote zilizozinduliwa mwaka uliopita. Kuna waimbaji wakubwa na waimbaji wadogo. Miongoni mwa waimbaji Watano wakubwa sana hapa Afrika mashariki mwaka uliopita kuna; Jose Chameleon, Diamond Platinumz, Sauti Sol, Bebe Cool na Eddy Kenzo. Waimbaji hawa wana nyimbo Chungu nzima. Nyimbo zao zote zinaburudisha, zinaelimisha na kufurahisha watu katika jamii. Mwimbaji mwenye nyimbo nyingi zaidi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni Bebe Cool. Ana nyimbo zaidi ya mia moja (100).

Mwimbaji maarufu sana nchini Tanzania na ni Diamond Platinumz. Nyimbo zake zinavuma sana hapa Afrika Mashariki na duniani kote. Fundi mitambo wa Diamond Platinumz anaitwa Master Jay na anasema kwamba Diamond ana nyimbo zaidi ya 50.

Watu wengi wanaenda kwenye matamasha, Kilabu na diskoni usiku kwa sababu wanataka kusikiliza na kucheza muziki mzuri wa waimbaji hao. Vijana wa siku hizi wavulana kwa wasichana wanajua kucheza muziki vizuri. Wasichana wanatingisha matiti na matako yao pamoja na sehemu nyingine za mwili. Wavulana wanarukaruka juu na chini huku wakichanganya miguu yao. Lakini kati ya wavulana na wasichana ni nani wanaojua kucheza vizuri zaidi? Muziki ni mzuri kwa kila mtu hata wakiwa watoto wadogo, vijana, wakubwa na wazee. Kwa kweli,Watu wote wanapenda muziki duniani. Wazee wengi wanataka sana kusikiliza muziki wa zamani, yaani ule muziki wa kipindi chao . Baadhi ya wazee wanapendelea sana muziki mwororo wenye mwendo wa polepole.

Ninaitwa Mukungu Collins. Mimi ni mvulana mwenye umri wa miaka kumi na Sita. Mimi ni mwananchi wa Uganda. Ninaishi mjini Kawempe, kaskazini mwa jiji la kampala. Mimi kama kijana wa kizazi kipya ninapendealea zaidi mziki wa Kijamaica maishani mwangu. Kuna waimbaji wakubwa wa kijamaica kama vile; Konshens, Busy Signal, Nicki Minaj, Bennie Man, Mr.Vegas, Patra, Tiana, Shaggy, Alaine, Kartel na Gyptian. Ni kweli kwamba Wajamaica wanaimba vizuri muziki wao wa aina ya reggae , ragga na dance hall.

Lakini mimi kama mpenda mziki, ninaona kwamba Wimbo mzuri wa mwaka

uliopita ulikuwa 'Kutama'! Wimbo huo umeimbwa na Fik Fameika. Mbali na wimbo huo, Mwanamziki huyo Fik Fameika ana nyimbo nyingine nyingi nzuri. Kwa mfano; Mbega wa baala, Gwe abisobola, Kachima, Mafia, Movie, Somebody, Mutuwulira, Property, Pistol , nakadhalika…

Hapa shuleni ninao Marafiki wengi sana ambao wanapenda mziki kama mimi. Wengi wao ninasoma nao Kiswahili katika kidato cha tatu. Miongoni mwa marafiki hawa ni; Twebaze, Agaba, Adinani, Bashir, Mutoni , Bukenya na katusiime . Tunapendana mno kama mlevi na pombe. Wanafunzi hao wanajua kuimba nyimbo na kucheza mziki wa kila aina. Tunacheza pamoja kwenye kikundi cha Nato katika Kilabu ya EAC. Wanajua kucheza Lingala, Hip-hop, B-Boy, Dance hall, RnB, nakadhalika..

***Maswali;..***

(a) Mwandishi wa habari hiyo ni nani? Je, ni mwananchi wa nchi gani?.

…………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………….

(b) Mwandishi ana umri wa miaka mingapi? Anasoma kidato cha ngapi?

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………….

(c) Mwandishi anapendelea zaidi muziki wa aina gani?

…………………………………………………………………………………

(d) .Wazee wanapendelea sana kusikiliza na kucheza muziki wa aina gani?

……………………………………………………………………………………

(e) Mwandishi pamoja na familia yake wanaishi wapi?

…………………………………………………………………………………….

f) Andika majina ya waimbaji wakubwa sana Afrika mashariki.

1……………………… 2………………………… 3……………………

4………………………… 5……………………

g) NI nani Mwimbaji mkubwa wa mwaka elfu mbili kumi na saba? Aliimba wimbo gani?

……………………………………………………………………………………..

h) Toa umuhimu wa muziki kwa watu katika jamii.

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

ii) Wewe kama mtoto wa kizazi kipya, unataka kucheza muziki wa aina gani?

……………………………………………………………………………………

j) Andika majina manne ya wanamuziki wako wakubwa wa kijamaica.

1…………………… 2…………………… 3………………… 4………………

k) i) Ni mwimbaji gani maarufu anayevuma sana nchini Tanzania?

……………………………………………………………………………………………

ii)Je, ana jumla ya nyimbo ngapi?

……………………………………………………………………………………

***©Idara ya Kiswahili 2020***